



Fedha za Kufufua Mikahawa

Sheria ya Marekani ya Mpango wa Kuokoa (American Rescue Plan Act) iliweka Fedha za Kufufua Mikahawa ili kutoa fedha za kusaidia mikahawa na biashara nyingine zinazofaa kubaki ikiwa wazi. Mpango huu unatoa fedha kwa mikahawa sawia na mapato waliyopoteza kwa sababu ya janga hadi dola milioni 10 kwa kila biashara lakini isiyozidi dola milioni 5 kwa kila eneo halisi. Wapokeaji hawahitajiki kulipa fedha hizi mradi wazitumie inavyofaa kufikia Machi 11, 2023.

Tembelea www.sba.gov/restaurants kwa habari zaidi.

Ni nani anaweza tuma ombi?

Biashara zinazofaa ambazo zimepoteza mapato kwa sababu ya janga zikiwemo:

- Mikahawa
- Vibanda vya chakula, malori ya kuuza chakula, mikokoteni ya kuuza chakula
- Wapishi wa vyakula katika sherehe
- Vilabu, mabaa, makumbi, migahawa
- Baa za kuuza vitafunio na vinywaji visivyo vileo
- Mahali au majengo yaliyo na leseni ya mtengenezaji wa vinywaji vilivyo na vileo ambapo umma inaweza kuonja, kuchukua sampuli, au kununua bidhaa
- Maduka ya kuokea mikate*
- Baa ya kutenezea pombe, vyumba vya kuonja pombe, vyumba vya bomba*
- Viwanda vya kutengenezea pombe na/au viwanda vidogo vya pombe*
- Viwanda vya divai na mitambo*
- Hoteli*

**Iwapo mauzo kwa umma inajumuisha angalau 33% ya risiti zote*

Jinsi na lini utakavyotuma ombi

Unawezatuma ombi kupitia washirika wa mikahawa halisi ya kuuza inayotambuliwa na SBA au moja kwa moja kupitia tovuti itakayopatikana katika <https://restaurants.sba.gov>.

SBA Unaweza kujiandikisha kwa taarifa yetu ya barua pepe kwa www.sba.gov/updates au tafuta akaunti zetu za mitandao ya kijamii kwa www.sba.gov/social-media.

Nyaraka zaidi zinaweza kuitishwa unapotuma ombi. Angalia orodha kamili kwa www.sba.gov/restaurants.

Pata usaidizi na ombi lako

Kwa usaidizi wa kutayarisha ombi lako, unaweza kutumia yafuatayo:

- Usaidizi wa kituo cha kupiga simu: 1-844-279-8898 (Saa: Jumatatu-Ijumaa 8 asubuhi-8 jioni ET)
- Ofisi ya SBA ya Wilaya yako kwa www.sba.gov/local-assistance
- Sampuli ya fomu ya ombi na mwongozo wa undani kuhusu mpango huu zinapatikana katika kugha mbalimbali kwa www.sba.gov/restaurants.